

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taasisi ya Benjamin William Mkapa inatekeleza Mradi wa Kuimarisha Mifumo Stahimilivu na Endelevu ya Afya (RSSH) kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya ngazi za vituo katika Mikoa kumi (10) iliyopewa kipaumbele na mradi huu ambayo ni Mwanza, Shinyanga, Mara, Simiyu, Geita, Kagera, Katavi, Tabora, Dodoma na Kigoma.

Hivyo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin William Mkapa inapenda kuwatangazia wahitimu wa kada za afya nchini kuwasilisha maombi ya nafasi za kazi, kuanzia **tarehe 20/01/2020** ili kujaza nafasi mbalimbali za Kada ya Afya katika Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati.

Nafasi zinazotangazwa ni zifuatazo:-

1. Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II

Waombaji wawe na Stashahada (Diploma) ya Uuguzi ya muda usiopungua miaka miwili kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

2. Muuguzi Daraja la II

Waombaji wawe na Cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kusajiliwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

3. Tabibu Daraja la II

Waombaji wawe na Stashahada (Diploma) ya Utabibu ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

4. Tabibu Msaidizi

Waombaji wawe wamehitimu Astashahada (Cheti) ya miaka miwili ya Tabibu Wasaidizi (Clinical Assistants Certificate) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

5. Mteknolojia Daraja la II (Maabara)

Waombaji wawe na Stashahada (Diploma) ya Sayansi ya Maabara ya muda wa miaka mitatu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na Mabaraza ya Taaluma.

6. Mteknolojia Msaidizi (Maabara)

Waombaji wawe wamehitimu Astashahada (Cheti) ya miaka miwili katika fani ya Maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza yao pale inapohusika.

SIFA ZA MWOMBAJI;

- i. Awe raia wa Tanzania;
- ii. Awe na umri usiozidi miaka 45;
- iii. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea;
- iv. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au asiwe Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali;
- v. Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini; na
- vi. Asiwe na check namba.

MAOMBI YOTE YAAMBATANISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:

- i. Barua ya maombi ya kazi ikieleza Mikoa mitatu ambayo mwombaji angependa kupangiwa kufanya kazi katika moja ya Halmashauri zake;
- ii. Nakala ya cheti cha kidato cha nne/sita;
- iii. Nakala za Vyeti vya Taaluma;
- iv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
- v. Nakala ya cheti cha usajili kamili (Full Registration) au Leseni ya kufanya kazi ya taaluma husika; na
- vi. Maelezo binafsi (CV), yakionesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/namba za kiganjani za wadhamini wasiopungua wawili.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE

- i. Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri yoyote watakayopangiwa ndani ya Mikoa kumi (10) ya mradi kama ilioainishwa hapo juu;

- ii. Waombaji waliosoma nje ya nchi wanatakiwa waambatanishe "Equivalent Certificate" kutoka NECTA/NACTE/TCU.

Maombi yote yatumwe kwa **njia ya mtandao (online)** kupitia mfumo wa kielektroniki unaopatikana kupitia anuani ya ajira.tamisemi.go.tz.

Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini hayatafanyiwa kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 7 Februari, 2020 saa 9:30 alasiri.

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya OR-TAMISEMI (www.tamisemi.go.tz) na tovuti ya Taasisi ya Benjamin William Mkapa (www.mkapafoundation.or.tz)

Tangazo Limetolewa na:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P 1923,
DODOMA.

20 Januari, 2020

